# HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILEMELA

*Mhe. Mwenyekiti na Wajumbe,*

*Baraza la Madiwani*

*Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela*

**YAH: TAARIFA YA MKURUGENZI KATIKA MKUTANO WA BARAZA LA MADIWANI KWA ROBO YA NNE (APRIL-JUNI) YA MWAKA WA FEDHA 2020/2021, TAREHE 20 AGOSTI 2021.**

## 1.0 UTANGULIZI

***Mhe. Mwenyekiti,*** Kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela za Mwaka 2014, Mkurugenzi anawajibika kulitaarifu Baraza la Madiwani juu ya Matukio mbalimbali ambayo yamefanyika au yanatarajia kutokea katika kipindi cha robo ya mwaka.

***Hivyo, taarifa hii itakuwa na mambo yafuatayo: -***

i. *Taarifa ya Ziara ya Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ya kutembelea wadaiwa sugu wa kodi ya Pango la Ardhi.*
ii. *Taarifa ya Ukaguzi Maalum (Special Auditing) wa Mapato na Miradi ya Maendeleo.*
iii. *Taarifa ya Upandishwaji wa Vyeo na Kubadilishiwa Muundo Watumishi.*
iv. *Taarifa ya Wanafunzi waliofanya Mitihani ya kuhitimu Kidato cha Sita kwa mwaka 2021.*



Scanned with CamScanner

v. *Taarifa ya Mapokezi ya Jumla ya Tsh. 399,200,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Elimu.*

vi. *Taarifa ya uzinduzi wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF III), Kipindi cha Pili.*

vii. *Taarifa ya Mkutano Maalum wa Baraza la Madiwani kwa ajili ya kupitia Hoja za Ukaguzi.*

viii. *Taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati ya "Stand" ya Mabasi na Maegesho ya Malori wa Nyamhongolo.*

## 2.0 UFAFANUZI WA TAARIFA

### *2.1.1 Taarifa ya Ziara ya Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.*

***Mhe. Mwenyekiti,*** Mnamo tarehe 17 Juni 2021, Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa Dk. Angeline S.L. Mabula alitembelea Manispaa ya Ilemela. Lengo la Ziara hiyo ilikuwa ni kutembelea wadaiwa sugu wa Kodi ya Pango la Ardhi, kujadili changamoto zao na kutafuta suluhisho kabla ya kuchukua hatua za kisheria dhidi yao.

Ujio huo ulikuwa ni sehemu ya ziara zake katika mikoa mbalimbali nchini kufuatilia makusanyo ya kodi ya pango la ardhi pamoja na kutatua changamoto zake.



Scanned with CamScanner

**2.1.2. Taarifa ya Ukaguzi Maalum (Special Auditing) wa Mapato na Miradi.**

**Mhe. Mwenyekiti**, Mnamo tarehe 24 Mei 2021, timu ya Wakaguzi kutoka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) walifika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kwa ajili ya Ukaguzi Maalum (Special Auditing) wa Mapato na Miradi mbalimbali ya Maendeleo.

Kazi hiyo ilifanyika kwa jumla ya siku 45 na taarifa ya Ukaguzi huo inatarajiwa kutolewa pamoja na taarifa ya Ukaguzi ya Mwaka 2020/2021.

**2.1.3 Taarifa ya Upandishwaji wa vyeo na Ubadilishaji wa Miundo kwa Watumishi.**

**Mhe, Mwenyekiti.** Mnamo tarehe 1 Mei 2021 wakati wa Maazimisho ya Kitaifa ya Sherehe ya Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi) yaliyofanyika katika Uwanja wa CCM-Kirumba uliopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan aliridhia zoezi la upandishaji wa vyeo na kubadilishiwa Muundo kwa watumishi wa Umma kote nchini kuanzia tarehe 1 Juni 2021. Hadi tarehe 30 Juni 2021, jumla ya taarifa za Watumishi 1407 (wanaostahili kupandishwa madaraja) wa kada mbalimbali wa Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela zilikuwa zimekwishaingizwa kwenye Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) na kwa mwezi huo huo wa Juni 2021, zaidi ya Watumishi 1,100



Scanned with CamScanner

walipokea mishahara mipya na ni matarajio yetu kuwa hadi ifikapo Mwezi Julai 2021 watumishi wote waliopandishwa madaraja watakuwa wamepokea mishahara mipya kadri inavyostahili.

### *2.1.4 Taarifa ya Wanafunzi waliofanya Mitihani ya Kidato cha sita Mwaka 2021.*

***Mhe. Mwenyekiti***, kuanzia tarehe 3 hadi 25 Mei 2021, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela kama ilivyo katika maeneo mengine nchini iliendesha zoezi la usimamizi wa mitihani ya kuhitimu kidato cha Sita. Jumla ya wanafunzi 786 (Me 213, Ke 573) waliweza kufanya mitihani hiyo katika jumla ya shule 9 zilizoko katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela. Matokeo ya Mitihani hiyo yanategemewa kutoka mapema Julai 2021.

### *2.1.5 Taarifa ya Mapokezi ya Jumla ya Tsh 399,200,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Elimu.*

***Mhe. Mwenyekiti***, Mnamo mwezi April 2021 Halmashauri yako ilipokea jumla ya Tsh. 399,200,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Elimu. Fedha hizi zilitoka Serikali Kuu kupitia program ya EP4R (Tsh. 320,000,000.00) na Tshs. 79,200,000.00 ni kupitia program ya COVID.

Fedha hizi zimepelekwa katika shule za sekondari za Sangabuye ambao wamepewa jumla ya Tshs. 80,000,000.00

kwa ajili ya ujenzi wa Bweni. Shule za Sekondari za Bujingwa, Nyamanoro na Kangaye walipata Tsh. 40,000,000.00 kwa kila shule kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa kwa kila shule. Shule za sekondari za Nyamanoro na Kirumba zilipewa Tsh. 13,200,000.00 kila moja kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo 12 katika kila shule.

Kwa upande wa Elimu Msingi, shule zilizonufaika na fedha hizi ni pamoja na Igogwe, Kaselya na Buswelu zilipokea Tsh. 40,000,000.00 kila moja kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa kwa kila shule wakati shule za Kaselya, Buswelu, Hekima na Tumaini zilipokea Tsh. 13,200,000.00 kila moja kwa ajili ya ujenzi wa matundu 12 ya vyoo kwa kila shule.

### *2.1.6 Taarifa ya uzinduzi wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF III) Kipindi cha Pili.*

***Mhe. Mwenyekiti***, mnamo tarehe 25 Mei 2021, Halmashauri yako ilizindua Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini (TASAF III) kipindi cha pili. Mpango huu pamoja na mambo mengine ulilenga kuandikisha (kutambua) kaya mpya zinazostahili kuwa kwenye Mpango kutoka katika Mitaa 74 ambayo haikuwemo kwenye Mpango hapo awali.

Katika zoezi la uorodheshaji (utambuzi), jumla ya Kaya 4437 ziliweza kuorodheshwa na kaya 3740 ziliandikishwa. Aidha kaya 697 kati ya 3740 zilizokuwa zimeandikishwa zilikosa sifa na hivyo kuondolewa kupitia mikutano ya hadhara ya Mitaa



Scanned with CamScanner

husika. Katika zoezi hili jumla ya Tsh. 56,000,000.00 ziliweza kutumika.

Aidha, katika kipindi hiki, Jumla ya Tshs. 154,632,000.00 zililipwa kwa kaya zinazoendelea kunufaika na Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini zipatazo 3,303.

### *2.1.7 Taarifa ya Mkutano Maalum wa Baraza la Madiwani kwa ajili ya kupitia hoja za Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.*

***Mhe. Mwenyekiti***, Mnamo tarehe 18 Juni 2021, Baraza lako lilikaa kupitia na kujadili hoja za Ukaguzi kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Katika Mkutano huo Maalum ambao pia ulihudhuriwa na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mheshimiwa Mhandisi Robert Gabriel, Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela mbali ya kuwa iliweza kupata hati safi ikiwa ni mara ya 5 mfululizo pia iliweza kupunguza idadi ya hoja kutoka hoja za ukaguzi 108 kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi hoja za ukaguzi 60 kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza aliipongeza Halmashauri kwa kuendelea kupata hati safi kwa mwaka wa 5 mfululizo na kusisitiza kuwa hoja zilizoibuliwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali zipatiwe majibu na vielelezo viwasilishwe haraka ili hoja hizo pia ziweze kufungwa.



Scanned with CamScanner

### 2.1.8 *Taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati ya "Stand" ya Mabasi na Maegesho ya Malori ya Nyamhongolo.*

***Mhe. Mwenyekiti,*** Halmashauri inaendelea na utekelezaji wa miradi miwili ya kimkakati ya Ujenzi wa Stendi ya Mabasi na Maegesho ya Malori katika eneo la Nyamhongolo kwa gharama ya Tsh. 27,095,103,464.00. Hadi sasa utekelezaji wa miradi hiyo umefikia asilimia 81% na Halmashauri imepokea jumla ya Tsh. 14,491,191,636.00 ambazo zimelipwa kwa Mkandarasi na Mtaalam Mshauri.

Maendeleo ya miradi yote kwa ujumla ni mazuri na mkandarasi yupo anaendelea na kazi kwa kasi nzuri. Mradi ulitarajiwa kukamilika ifikapo Mei, 2021 lakini kutokana na changamoto ya ucheleweshaji wa malipo kwa mkandarasi, muda wa ukamilishaji umeongezeka hadi Septemba 2021.

***Mhe. Mwenyekiti,*** *naomba kuwasilisha.*

Eng. Modest J. Apolinary
**MKURUGENZI WA MANISPAA**
**ILEMELA**



Scanned with CamScanner